(2) Mtu ambaye amesajiliwa kuwa mwezeshaji wa watoa huduma za usafiri ardhini hatoenda kinyume na masharti yaliyowekwa kwenye cheti cha usajili.

(3) Usajili utakapotolewa hautoweza kuhamishwa.

Mapitio
TS. Na. 73 ya mwaka 2020

19. Mtu ambaye hataridhika na maamuzi ya Mamlaka atatuma maombi ya mapitio kulingana na Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Utaratibu wa mapitio) za mwaka 2020.

Rufaa
Sura 413

20. Mtu ambaye atakuwa hajaridhika na maamuzi ya Bodi chini ya Kanuni hizi anaweza kukataa rufaa kwenye Tume ya Ushindani ndani siku kumi na nne toka tarehe ya maaamuzi.

1. Maombi ya kwanza lazima yaambatane na vitu vifuatavyo:
   a) Nakala halali ya leseni ya biashara;
   b) Nakala ya umiliki wa ofisi au makuabaliano ya pango;
   c) Cheti cha kodi;
   e) Nakala ya kitamulisho cha Uraia kwa mtu binafsi au cheti cha usajili kwa kampuni;
   f) ikiwa ni wakala wa basi atapeleka nakala ya makuabaliano ya huduma ya muendeshaji;

   Nyaraka zingine za ziada kwa kampuni
   (a) nakala ya cheti cha usajili wa kampuni;
   (b) cheti cha mlipa kodi cha sasa;
   (d) nyaraka zinginezo Mamlaka itakazohitaji muda wowote.

2. KUHUISHA
   (a) uthibitisho wa malipo ya tozo ya Mamlaka kwa mwaka uliotangulia;
   (b) nyaraka zingine Mamlaka inaweza kuhitaji muda wowote.

Mimi/ Sisi tunaapa kwamba kwa akili zetu/zangu timamu naamini kuwa taarifa nilizotoa/ ulizotoa kwenye maombi haya ni ukweli mtupu.

Jina Kamili ………………………………... Sahihi: ………………………...

Wadhifa: ………………………………. Tarehe: ……………………………..

KWA MATUMIZI YA OFISI

4. Uhakiki na Uidhinishaji
   (a) Haijaidhinishwa:
   Toa sababu
   …………………........……….
   (b) Imeidhinishwa:
   Tarehe ya kuanza:
   ………………………………….
   Tarehe ya mwisho:
   ……………………......

   Jina kamili la afisa:

